KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 15, Issue 1

9th Dhul Qa'dah 1432

7th Oct, 2011

YALIYOMO

YA'JUJ NA MA'JUJ 1

'ISSA IBN MARYAM 3 - 4

YA'JUJ NA MA'JUJ Na: Sheikh A. Hijazi (حفظه الله)

Allaah (سبحانه وتعالى) ametaja katika Qur'an kuhusu kisa cha Jooj wa Ma'jooj, ambao waliozuiwa nyuma ya Bwawa: **"HATA WATAKAPOFUNGULIWA YAAJUJ NA MAAJUJ WAKAWA WANATEREMKA KUTOKA KILA MLIMA (HAPO KIYAMA KITAKUWA TAYARI). NA ITAFIKA ILE AHADI YA HAKI.** [al-Anbiyaa 21: 96-97].

Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Ya'juj na Ma'juj huchimba mitaro kwenye Bwawa kila siku mpaka hukurubia kufikia kuuona muangaza wa jua, pindi kiongozi wao anapowaambia, "Haya rudini sasa! Mutakuja kuendelea kuchimba kesho.' Hatahivyo, Allaah huujenga tena ukawa na nguvu zaidi kuliko ulivyokuwa hapo awali. Watakapofika katika wakati unaotakiwa na Allaah atakapoamuru kuwapeleka kwa watu, watakuja (walichimbe Bwawa) mpaka wawe ni wenye kuuona muangaza wa jua. Kisha, kiongozi wao atasema, 'Haya rudini sasa! Mutakuja kuendelea kuchimba kesho, Insha-Allaah.' Watarudi na watalikuta (bila ya mabadiliko yoyote) kama walivyoliacha (katika siku ya) jana yake na wachimbe mpaka watokeze kwa binadamu. Watayanywa maji na watu watatafuta hifadha kutokamana na wao kwenye ngome zao. Watavurumiza mishale yao angani; wataregea na kitu mfano wa damu iliyokauka kwenye miili yao kisha waseme, 'Tumewashinda watu wa ulimwenguni na kuwatawala wakaazi wa mbinguni, kisha Allaah atawaletea* ***An-Naghaf*** *kwenye shingo zao ambao ndiwo watakao wauwa. Naapa kwa Yule ambae Aliyeimiliki roho yangu! Wanyama wa ardhini watanenepa na kuvimbishwa na maziwa kutoka kwenye nyama zao na damu."* [Ahmad, Abu Daawud na al-Haakim, Swaheeh al-Jaami' as-Swagheer no. 2276].

Ya'juj na Ma'juj watapita kwenye bahari ya Galilee na watakunywa maji yake yote kama ilivyopokewa katika hadeeth ya an-Nawaas Bin Sam'aan. Vilevile Allaah atampelekea wahyi Mtume wake 'Issa (عليه السلام), mwana wa Maryam awakusanye waumini kwenye mlima wa at-Tur kwa sababu hakuna binadamu awezae kuwashinda Ya'juj na Ma'juj. Kisha atawaangamiza kwa kuwaletea sampuli fulani ya minyoo itakayotokeza kwenye vishogo vyao, na watakufa kwa urahisi na haraka utadhani ni nafsi moja inayokufa.

Amepokea Abu Sa'eed al-Khudhree' (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Ya'juj na Ma'juj watawachwa wawavamie wanaadamu, kama Allaah alivyosema:* ***"WAKAWA (HAO YA'JUJ NA MA'JUJ) WANATEREMKA KUTOKA KILA MLIMA."*** [al-Anbiyaa 21: 96-97].

Watawatenza watu nguvu. Waislamu itawabidi watafute hifadha kwenye miji yao na ngome zao, wao pamoja na wanyama wao. Ya'juj na Ma'juj watayanywa maji ya katika ardhi. Hata baadhi yao watapita kwenye mto na watakunywa mto mzima mpaka wauwache ukiwa umekauka. Yoyote atakaekuwa nyuma yao atapita kwenye mto na aseme, 'Hapa paliwahi kuwa na maji!' Hapatowachwa mtu yoyote isipokuwa atakuwa ni mwenye kutafuta hifadha kwenye mji au ngome. Mmoja wao atasema, 'Hao ni watu ulimwenguni, tushamalizana nao. Sasa wamebaki wakaazi wa Mbinguni peke yao!' Kisha mmoja wao atautingisha mkuki wake na autupe mbinguni na utarudi ukiwa na damu. (Yote haya yatakuwa kama) mtihani na fitnah (kwa wanaadamu). Watakapokuwa wakifanya haya, Allaah atawaletea viumbe mfano wa Minyoo ya Parare watakaowaganda kwenye shingo zao, mpaka wafe kifo cha parare, wakiwa wamelaliana mmoja juu ya mwengine. Kutakapopambazuka asubuhi, Waislamu hawatosikia sauti zao. Kwahivyo, Waislamu watasema, 'Ataweza mtu kujiuza nafsi yake (kwa ajili ya Allaah) akajionee yaliyowasibu?' Kisha mtu mmoja miongoni mwao atashuka awaendee akiwa na hakika yakwamba watamuuwa. Atawakuta wamekufa wakiwa wamelaliana mmoja juu ya mwengine. Atapiga mayowe kwa Waislamu wenzake, 'Khabari njema! Adui yenu ameangamizwa.' kisha watu watajitokeza na kuwafungulia wanyama wao. Hapatokuwa na nyasi za malisho lakini ni maiti watupu. Watanenepa kutokana kuwala wao kuliko walivyowahi kutokana na kula aina yoyote ya mti wowote.'" [Ibn Maajah, Swaheeh Sunan Ibn Maajah, no. 3297]

Katika hadeeth ya an-Nawwas Bin Sam'an, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kisha, 'Issa* (عليه السلام), Mtume wa Allaah atashuka pamoja na Maswahaba zake kwenye sehemu ya chini ya ardhi. Watakuta hapana nafasi ya hata msamba mmoja isipokuwa kumeenea mafuta yao na muozo (wa mati zao). 'Issa Mtume wa Allaah na Maswahaba zake watamuomba Allaah Du'aa'. Basi Allaah atawaleta Ndege wakubwa kiyasi cha shingo za Ngamia, watakaowabeba (maiti za Ya'juj na Ma'juj) na watakwenda kuwatupa popote apendapo Allaah. Kisha, Allaah ataleta mvua itakayonyesha juu ya kila nyumba ya udongo (au mawe) au manyoya ya kila mnyama, itakayosafisha ardhi mpaka ing'are kama kiyoo. Ardhi itaamrishwa, 'Toa matunda yako na urudishe baraka zako." Huu ndio wakati ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) alousifu kwa kusema: *"Maisha yaliyobarikiwa ni ya baada ya Maseeh."* Vilevile, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alieleza kuhusu idadi ya Ya'juj na Ma'juj aliposema: *"Waislamu watatengeza moto kwa kutumia mishale na mikuki ya Ya'juj na Ma'juj kwa miaka saba."*

ALAMA NYENGINE KUBWA ZA KIYAMA

Na Sheikh A. Hijazi

Hadeeth ya an-Nawwas Bin Sam'an imesimulia yakwamba upepo msafi wa kuzizima utasambaa juu ya ardhi na kunasa roho za kila mu'min na Muislamu. Baadae watabaki watu waovu peke yao juu ya ardhi hii na watajishughulisha na kila sampuli ya uharibifu, pakiwemo uzinifu hadharani. Na muda mchache tu kabla ya kuja upepo huu, jua litachomoza kutoka upande wa Magharibi, mnyama atakaechipuza kutoka ardhini atazungumza moja kwa moja pasi na kizuizi na watu; Qur'an itafutwa kutoka vitabuni na kutoka nyoyoni mwa watu; Sheriya za Uislamu zitaachiliwa mbali na moshi mkubwa utaimeza ardhi. La mwisho katika alama hizi ni moto utakaotoka katika sehemu za chini ya Aden, mahali fulani huko Yemen.moto huu utawachunga watu kutoka Mashariki hadi Magharibi, kuelekea kwenye ardhi zao za mkusanyiko huko Ash-Sham, na hautowacha kuwa nao hadi wafike mwishoni mwa kikomo chao.

Hadeeth hiyo haitoi maelezo zaidi kuhusiana na mitetemeko mitatu itakayosababisha ardhi ibomoke, isipokuwa kwa mtetemeko karibu na Madinah utakaowatia wasiwasi jeshi litakaloelekea Makkah kutaka kumuuwa al-Mahdi. Huu hwenda ukawa ni mmojawapo wa mitetemeko mitatu. Hatahivyo, Allaah ndiye Mjuzi zaidi.

Hudhaifah Bin Usaid al-Ghifari amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitupitia tulipokuwa tukizungumza na akasema: 'Ni yapi muyazungumzayo?' wakajibu: 'Sisi twazungumza kuhusu Kiyama.' Akasema: 'Hakitokuja hadi muone alama kumi kwanza.' kisha akata ad-Dukhaan (moshi); ad-Dajjaal, Mnyama; kuchomoza kwa jua kutoka Magharibi; kushuka kwa 'Issa, mwana wa Maryam; Mitetemeko mitatu [ambapo ardhi itakapobomoka]; moja katika upande wa Mashariki, moja katika upande wa Magharibi, na mmoja katika Bara Arabu. La mwisho ni moto utakaowaka kutoka Yemen ukiwachunga watu kuelekea kwenye kikomo chao cha ardhi ya mkusanyiko. [Muslim, Sharh an-Nawawee 'ala Swaheeh Muslim, vol. 18, Uk. 27]

KUCHOMOZA KWA JUA KUTOKA MAGHARIBI

Amesema Allaah**: "WANANGOJA JENGINE ILA WAWAFIKIE MALAIKA (KUWATOA ROHO) AU IWAFIKIE (ADHABU KAMILI YA) MOLA WAKO, AU ZIFIKE BAADHI YA ISHARA ZA MOLA WAKO (ALIZOSEMA KUWA ZITAWAFIKIA)? SIKU ZITAKAPOFIKA BAADHI YA ISHARA ZA MOLA WAKO, BASI MTU (KAFIRI) HAITAMFAA IMANI YAKE, AMBAYE ALIKUWA HAKUAMINI ZAMANI, AU (MWISLAMU) HAKUCHUMA KHERI KATIKA UISLAMU WAKE. SEMA: 'NGOJENI, SISI PIA TUNANGOJA.' [al-an-'Aam 6:158].**

Imaam Muslim amepokea yakwamba Abu Dharr amesema, "Siku moja Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: 'Mwajua Jua linakwenda wapi? Wakajibu, 'Allaah na Mtume wake ndio wajuzi zaidi. Akasema, 'Linakwenda mpaka lifike kwenye njia iliyowekewa chini ya 'Arsh na likasujudu na kuendelea kufanya hivyo mpaka litakapoambiwa, 'Inuka! Rudi kule utokako. Lirudi na kuchomoza asubuhi kutoka katika mahali linapochomoza kwa kawaida yake. Kisha, haliyakuwa watu hawatoshuku lolote, litakwenda mpaka lifike kwenye njia yake chini ya 'Arsh, litaambiwa, 'Inuka! Chomoza kutoka kule unapozama.' Basi litachomoza kutoka Magharibi.' Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema, 'Munajua haya yatatokea lini? Haya yatatokea katika wakati ambapo hapana nafsi itakayofaidika kutokana na Imani yake, isipokuwa iwapo imeamini kabla na kupata faida kutokana na Imani yake.'" [Muslim, Sherh an-Nawawee 'ala Swaheeh Muslim, vol. 1, Uk. 169].

MLANGO WA MSAMAHA UTAKUWA WAZI MPAKA JUA LITAKAPOCHOMOZA KUTOKA MAGHARIBI

Safwaan Bin 'Assal amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema, "Kuna mlango ulio wazi, wenye upana wa miaka sabiini, katika upande kunapokutwa Jua. Mlango huu utaendelea kuwa wazi kwa ajili ya kupokea msamaha mpaka Jua litakapo chomoza kutoka katika sehemu linapokutwa. Litakapochomoza kutoka hapo, hapana nafsi itakayofaidika kutokana na Imani yake, mpaka iamini kabla ya hapo na kufaidika na jema lolote kutokana na Imani yake." [Ibn Maajah, Swaheeh Sunan Ibn Maajah, no. 3289].

Vilevile Abu Hurairah amesema, "Nimemsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema, 'Kiyama hakitokuja mpaka Jua lichomoze kutoka katika sehemu linapokutwa. Litakapochomoza kutoka katika sehemu linapokutwa, na watu watakaposhuhudia hayo, wote wataamini. Hatahivyo, huo ndio wakati ambao hapana nafsi itakayofaidika kutokana na Imani yake, isipokuwa iwe imeamini kabla ya hapo na kufaidika na wema kutokana na Imani yake.'"

MNYAMA

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"NA KAULI (YA KUJA KIAMA) ITAKAPOWATHIBITIKIA TUTAWATOLEA MNYAMA KATIKA ARDHI ATAKAYEWASEMEZA KWA SABABU WATU WALIKUWA HAWAZIYAKINISHI AYA ZETU."** [an-Naml 27: 82].

Amesema Abdullaah Ibn 'Umar, "Mimi nimeihifadhi hadeeth kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambayo sijaisahau. Nimemsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: *'Alama ya kwanza itakayokuja ni kuchomoza kwa Jua kutoka katika sehemu linapokutwa na watu watakapotokezewa na Mnyama katika wakati wa mapambazuko. Lolote litakalotokea katika mawili haya kabla ya jengine, basi jengine halitokuwa na muda nalo litafuata."* [Muslim, Mukhtasar Swaheeh Muslim, no. 2053].

Mnyama atatokeza kutoka kwenye ardhi, akiwapiga mihuri watu kwenye pua zao, (yanayosomeka);

"... Huyu ni mu'min na huyu ni Kaafir."

Mpaka upepo msafi ulio na mzizimo utakapokuja na kuchukuwa roho za kila Mu'min na kila Muislamu.

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم)*: "Mnyama atatokeza na atawapiga mihuri watu juu ya pua zao. Kisha atabaki na nyinyi mpaka mtu atakapomnunua mnyama na akauliozwa, 'Umemnunua kutoka kwa nani?' atajibu, 'Kutoka kwa mtu aliyepigwa muhuri."* [Ahmad, Swaheeh ul Jaami' as-Swagheer, no. 2927].

MOTO UTAKAOWAKUSANYA WATU

Moto utakaowakusanya Binadamu wote kwa siku ya Malipo ndiyo alama ya mwisho katika alama kumi kubwa. Moto huo utaanzia Yemen, kutoka katika sehemu za chini za Aden, na utakuwa ukiwachunga watu, "Ukiweka kambi pale watakapoweka kambi, na utapumua pale watakapopumua." [Sherh an-Nawawee 'ala Swaheeh Muslim, vol. 18, Uk. 29].

Kabla ya kuja kwa Moto uwakao na upepo msafi wenye mzizimo, 'Uislamu utapotea kama ambavyo urembo wa

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

nguo unavyopotea. Mpaka iwe hakuna tena kufunga saumu, hakuna kuswali, hakuna kuchinja wala kutoa zaka na swadaka kutakako kuwepo. Kitabu cha Allaah kitafutwa kunako usiku mmoja na wala hakutobaki hata aya moja juu ya ardhi hii. Makundi ya wazee, wake kwa waume, watakuwa wakisema 'Tulikuwa tukiwaona wazee wetu wakitamka neno hili *LAA ILAAHA ILLALLAAH', basi na sisi tunatamka hayo."j* [al-Haakim, al-Mustadrak, vol.4, Uk. 473. na akasema yakwamba ni swaheeh kulingana na masharti ya Muslim]. Hatahivyo, baada ya upepo msafi wenye mzizimo kuzinyakuwa roho za waumini na Waislamu, watu watarudi kwenye ibada za masanamu na vijiungu vyengine, kama walivyokuwa wakifanya wazazi wao katika zama za Jaahiliyyah. Amepokea Imaam Muslim yakwamba 'Aaisha amesema: "Nimemsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema, *'Mchana na Usiku haitomalizika mpaka al-Laat na al-'Uzza waabudiwe tena!'* Nikasema, 'Yaa Rasoolullaah, mimi nilidhania yakwamba Allaah alipoteremsha aya isemayo, **"YEYE NDIYE ALIYEMTUMA (ALIYEMLETA) MTUME WAKE (NABII MUHAMMAD) KWA UONGOFU NA KWA DINI YA HAKI ILI KUIFANYA ISHINDE DINI ZOTE, IJAPOKUWA WASHIRIKINA WATACHUKIWA."** [as-Swaaf 61:9]. Kutaimarika kwa kutadumu maisha?' Akasema, Hili litakuwepo mpaka apendapo Allaah, kisha ataleta upepo mzuri utakaomletea mauti kila mwenye chembechembe ya Imani kwenye moyo wake. Baada ya hapo, watabaki wale wasiokuwa na wema peke yao na watarudi kwenye dini za wazee wao.'" [Muslim, Mukhtasar Swaheeh Muslim, no. 2013].

Vilevile Abu Hurairah amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *Kiyama hakitokuja mpaka wanawake wa kabila la al-Daws watakapotingisha sehemu zao za nyuma kwa kumzunguka Dhil-Khalasah [Sanamu ambaye kabila la Khuza'ah waliekuwa wakimuabudu kabla ya Uislamu]."*

NI KINA NANI WATAKAOKISHUHUDIA KIYAMA

Kiyama kitashuhudiwa na wale wasiojua wema wa aina yoyote au Imani. Allaah amekwisha kuamuru yakwamba hakitoanza awapo Mu'min yoyote atakuwepo juu ya ardhi hii. Hii ndiyo sababu kitaanza juu ya wale walio waovu pasipo na shaka yoyote, wale wasioarisha wema wala wasiokataza maovu, wale wasiojua wema wala kukataza maovu. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kiyama hakitoanza isipokuwa juu ya waovu zaidi miongoni mwa viumbe."* Pia Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kiyama hakitoanza mpaka hapana atakaesema, 'Allaah, Allaah'.* Kwa maana yakwamba hapana atakaesema, "*LAA ILAAHA ILLALLAAH",* kama ilivyopokewa kwenye hadeeth iliyo swaheeh iliyopokewa na Imaam Ahmad. Vilevile amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) : *"Kiyama hakitoanza haliyakuwa mtu atakuwa akimkama Kondoo jike Maziwa. Lakini hatahivyo, bakuli (la maziwa) halitofika mdomoni mwake mpaka (Kiyama) kianze." Watu wawili watakaoshughulika kwenye biashara na ununuzi wa nguo—hawatomaliza mapatano yao ya kibiashara, lakini (kiyama) kitaanza. Mtu atatengeneza chombo chake (cha kuwanywesha Ng'ombe wake), na hatoweza kuwaleta kunywa, lakini (kiyama) kitaanza." Hebu fikiria jinsi watu walivyo ni wenye kusahau kuhusu mambo magumu ya Siku ya Kiyama na Siku ya Kufufuliwa, haliyakuwa* Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema."*Vipi mimi nitakuwa ni mwenye kuishi na starehe, haliyakuwa mshika tarumbeta ameshaiweka mdomoni mwake, na kuinamisha kichwa chake, akiwa anasikiliza kwa makini, anasubiri kuamrishwa aivuvie, ili nae aivuvie?"* Wakasema Waislamu, "Yaa Rasoolullaah! Tusemeje?" Akasema, *"Semeni, Hasbunallaah wa Ne'mal Wakeel, Tawakkalnaa 'alallaah Rabbinaa."*

Katika Hadeeth nyengine, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Tangu alipopewa majukumu yake, macho ya mshika tarumbeta yako tayari na ameyanyanyua kuangalia 'Arshi, kwa kuchelea yakwamba iwapon atapoteza maono yake, huwenda akaamrishwa (aipulize tarumbeta yake). Macho yake ni kama Sayari mbili zenye kung'ara."*

Sisi twasema, "Hasbunallaah wa Ne'mal Wakeel." Mategemezi yetu yote ni kwa Allaah, Mola wetu.

Twamuomba Allaah Atuhifadhi na atusalimu salama kutokamana na Vitisho vya Siku Kubwa ya kutisha, **"SIKU AMBAYO HAYATAFAA MALI WALA WATOTO, ISIPOKUWA MWENYE KUJA KWA ALLAAH NA MOYO SAFI."** [ash-Shu'araa' 26: 88-89].

'ISSA (عليه السلام) MWANA WA MARYAM

Allaah (سبحانه وتعالى) aliwakosoa Mayahudi katika madai yao yakwamba walimsulubu Mtume 'Issa, mwana wa Maryam, akasema: **"Na kwa (ajili ya) kusema kwao: 'Sisi tumemuuwa Masihi 'Issa, mwana wa Maryamu Mtume wa Allaah,' hali hawakumuuwa wala hawakumsulubu, bali walibabaishiwa (mtu mwengine wakamdhani nabii 'Issa). Na kwa hakika wale waliokhitalifiana katika (hakika) hiyo (ya kumuuwa Nabii 'Issa) wamo katika shaka nalo (jambo hilo la kusema kauwawa). Wao (kabisa) hawana yakini juu ya (jambo) hili (la kuwa kweli wamemuuwa Nabii 'Issa), isipokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumuuwa. Bali Allaah alimnyanyua kwake, na Allaah ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima."** [an-Nisaa' 4:157-158].

"(Kumbukeni) Allaah aliposema: 'Ewe 'Issa! Mimi nitakutimizia muda wako wa kuishi (hawatakuuwa hao maadui). Na nitakuleta kwangu, na nitakutakasa na wale waliokufuru (hawataweza kukudhuru) ..."

Kwahivyo, 'Issa (عليه السلام) hakuuwawa wala hakusulubiwa na atakuja kwenye ardhi hii kwa mara ya pili kuja kupigana na makafiri na awalazimishe waukubali Uislamu. Baadhi ya watu wa Kitaab watamuamini, kama alivyosema Allaah: **"Na hakuna yoyote katika watu waliopewa Kitaab (Mayahudi na Manaswara) ila humwamini (Nabii 'Issa kwa hakika yake) kabla ya kifo cha kila mmoja katika hao. (Lakini hakuna faida kumwamini huko wakati huo). Naye (Masihi) siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao."** [an-Nisaa' 4: 159].

Hadeeth ya an-Nawwaas Ibn Sam'an imeeleza kuwa 'Issa mwana wa Maryam atashuka kwenye Mnara mweupe katika sehemu ya Mashariki mwa Damascus. Hadeeth hiyohiyo pia imetaja yakwamba kafiri yoyote ambaye pumzi za 'Issa zitakaemfikiya ataangamia na pumzi zake zitafika kwenye upeo wa maono yake yanapofika. Pia tumetaja yakwamba ad-Dajjaal atauwawa na mkono wa 'Issa (عليه السلام).

UMBILE LA 'ISSA NA KAZI YAKE ATAKAPOKUJA KWA MARA YA PILI

Amepokea Ibn Abbaas yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Katika Usiku wa al-Israa', nilipita kwa Musa* (عليه السلام)*, mwana wa 'Imraan, na nikamuona ngozi yake ni ya kahawiya*

(Continued from page 3)

iliyokolea, alikuwa ni mrefu na mwenye nywele za mapindo na amekaa kama jamaa za Shanoo'ah (kabila fulani la Yemen). Na nikamuona 'Issa mwana wa Maryam; alikuwa na mwili uliojaa vyema, (na rangi ya ngozi yake ilikuwa) baina ya nyekundu na nyeupe na nywele zake zilikuwa ni nyororo."

Vilevile, Imaam Muslim amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Niliwekewa Mitume mbele yangu kwa ukaguzi (katika usiku wa al-Israa') na nikakuta yakwamba Musa alikuwa ni mtu mfano wa jamaa za Shanoo'ah. Pia nikamuona 'Issa* (عليه السلام)*, mwana wa Maryam na nikakuta yakwamba mtu anaefanana nae ni 'Urwah Bin Mas'ud. Alikuwa na mwili uliojengeka vyema, rangi yake ilikuwa ni nyekundu kana kwamba anatoka kwenye bafu kuoga hivi sasa." Abdullaah Ibn 'Umar, amepokea kuwa* Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Katika usiku mmoja nilijikuta kwenye Ka'bah, mara nikamuona mtu mwenye rangi ya ubichi, alikuwa ni mzuri kama alivyo mtu mwenye rangi yenye ubichi kwa waume ilivyo, na nywele zake mpaka kwenye masikio, zilikuwa ni nywele nzuri ziso-kifani. Alizichana zikawa zinadondoka maji. Alikuwa amejiegemeza juu ya watu wawili—au juu ya mabega ya watu wawili—wakizunguka Ka'bah. Nikauliza, 'Huyu ni nani?' Nikajibiwa, 'Huyu ni Maseeh, Mwana wa Maryam ..."*

Vilevile, amepokea Abu Hurairah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hapakuwa na Mtume baina yangu mimi na 'Issa nae atateremka, na atakapoteremka, basi mjueni. Ni mtu aliye na mwili uliojaa vyema kabisa, (rangi ya ngozi yake) ni baina ya nyekundu na nyeupe. Atateremka akiwa amevaa vipande viwili vya kitambara. Kichwa chake ni kama chenye kudondoka maji ingawaje hapakuwa na umande wa hali ya anga uliomgusa. Atawapiga watu vita waukubali Uislamu, avunje misalaba, awauwe Nguruwe na awawekee al-Jizyah. Katika zama zake, Allaah ataziangamiza dini zote isipokuwa Uislamu na amuangamize al-Maseeh ad-Dajjaal. Maseeh ('Issa) atabaki kwa miaka arubaini katika ulimwengu huu, kisha atakapokufa, Waislamu ndio watakaomswalia."*

Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameeleza wakati ambapo 'Issa atakaposhuka, kazi yake na hali ya Waislamu hapo. Akasema, *"Na Imaam wao atakuwa ni mtu mwema. Atakaposongea mbele (Imaam wao) kuwaswalisha watu, 'Issa mwana wa Maryam ndipo atakapowashukia asubuhi. Imaam huyo atarudi nyuma ili ampishe 'Issa asonge mbele. Hatahivyo, 'Issa ataweka mkono wake baina ya mabega yake na kisha amwambie, 'Songea mbele na uswalishe, kwani swala iliwekwa kwa ajili yenu (kuiongoza)'. Imaam wao atawaongoza kwenye swala hiyo. Atakapo ondoka 'Issa atasema, 'Fungueni Mlango', wataufungua haliyakuwa ad-Dajjaal, pamoja na jeshi lake la Mayahudi Elfu sabiini, wote wakiwa wamejivalia majambia yaliyorembeshwa maridadi na ala zake, watakuwa nyuma ya Mlango huo. Ad-Dajjaal atakapomuangalia, atayayuka kama inavyoyayuka chumvi kwenye maji na ataanza kukimbia. ('Issa ataanza kumfukuza na) atamshika karibu na Mlango wa Mashariki wa Lud na amuuwe. Kisha Allaah atawagharakisha Mayahudi wasipate pa kukimbilia popote ambapo alipoumba Allaah. Kila kitu, iwapo ni jiwe, mti, ukuta au mnyama—isipokuwa Mti aina fulani, kwa sababu ni mmojawapo wa miti yao, vitaja'aliwa na Allaah kuzungumza, vikisema, 'Ewe Mja wa Allaah, Ewe Muislamu! Yahudi huyu hapa, njoo umuuwe. 'Issa, mwana wa Maryam atakuwa ni kiongozi muadilifu na Imaam aliye juu ya usawa, atavunja misalaba, awauwe Nguruwe, alipishe al-Jizyah, na matokeo yake ni kwamba hapatokuwa na Ngamia wala Kondoo watakaochungwa. Migogoro yote chuki zitatokomea na (wanyama) wote wa hatari hawatokuwa na madhara. Hata kijana mchanga atacheza na nyoka na wala hatomdhuru. Kijana cha kike atamdhuru Simba na wala Simba asimdhuru kwa chochote. Mbwa mwitu atakuwa kama Mbwa mlinzi kwa Kondoo. Amani itaenea kwenye ardhi nzima, kama chungu kilichojaa maji. Neno litakuwa ni moja tu, na ataabudiwa Allaah Peke yake. Hapatokuwa tena na vita na utaondolewa utawala wa Quraish. Ardhi itakuwa kaka chungu cha fedha, na majani yake yatamea kama yalivyokuwa katika zama za Adam. Hata kundi (la watu) watakusanyika kwenye kishada cha zabibu na watakila mpaka washibe . Na kundi la watu watalikusanyikia komamanga, liwashibishe wote. Thamani ya Ng'ombe itakuwa ni kadhaa na kadhaa, na thamani ya Farasi itakuwa ni dirham chache tu.*

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]

THE QUR'AN & SUNNAH HAJJ / 'UMRAH AGENCY

1432HIJRI/ 2011 C.E

Assalaamu 'Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah mwaka huu 1432 Hijri/ 2011, tumeanza Barnaamij ya kupeleka watu Hajj.

Mipangilio Ya Safari

- Kuondoka ni katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Dhul Qa'dah
- Kurudi ni mwisho wa mwezi wa Dhul-Hijjah
- Safari itaanza Mombasa – Nairobi – Jeddah
- Kurudi ni Jeddah – Nairobi – Mombasa
- Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli, Usafiri na Chakula – mara 3 kwa siku tukiwa Mina kwa siku tano)
- Class "B" ni $3800 U.S Dollars / Class "C" ni $3200 U.S Dollars
- Amma mas'ala ya Chakula (Makka na Madinah) kila mtu ni juu yake
- Tutakuwa na Darsa juu ya mas'ala ya Hajj kabla ya kuondoka na tutakapokuwa Makkah
- Tutaandamana na Daktari wetu kutoka hapa Mombasa Insha Allaah

Kwa Maelezo Zaidi

Fika katika Maktaba ya QSS iliyoko ubavuni mwa Tajj Hotel (Duka la tatu baada ya Duka la vitabu vya Dini), au

Wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net, au

Tupigie simu nambari mojawapo ya hizi zifuatazo:

+254 723471820 au +254 721473181, au +254 700365253